

MAJILIO 2026 – WIKI YA 3

SHUHUDIENI!

Kuuelekeza Ulimwengu kwenye Nuru

Yohana 1:6–9; 19–28



**“Malaika akawaambia, Msiogope;
kwa kuwa mimi ninawaletea habari
njema ya furaha kuu itakayokuwa
kwa watu wote”**

Luka 2:10 (SRUV)



Leo tunawasha mshumaa wa FURAHA.

Yohana alikuja kuwa shahidi wa Nuru.
Sisi pia tumeitwa kufanya vivyo hivyo.



Furaha inazidi kudhihirika
katika ubatizo, mikusanyiko ya ibada na
shuhuda za maisha yaliyobadilishwa.



**Tunawasha mshumaa huu kwa ajili ya
nyimbo za furaha zinazoimbwa katika
makanisa kote ulimwenguni,**

**kwa ajili ya waumini wapya, wamisionari, na jumuiya
ambako kukata tamaa kunabadilishwa kuwa tumaini.**



**Tuwe watu wanaoileta furaha
hiyo ulimwenguni;**

furaha inayoponya, furaha inayorejesha,
na furaha inayowaalika wengine kumjua Yesu.



**Mungu wa furaha,
tunakushukuru kwa habari njema
zinazoleta nuru kwa kila taifa.**

Furaha yako ifurike ndani yetu na kupitia kwetu. Liimarishe Kanisa
lako ili tuwe mashahidi wenye furaha, hata katikati ya mateso.
Mshumaa huu utukumbushe kwamba furaha yako ni kwa ajili ya
watu wa mataifa yote.

Amina.



